



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**



**TAARIFA KWA UMMA  
TANGAZO LA FURSA YA MAFUNZO YA UKUZAJI UJUZI**

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) inatekeleza mradi wa Ukuzaji Ujuzi nchini kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Chama Cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho La Vyama vya Wafanyakazi Denmark (DTDA) pamoja na Shirikisho la wenye Viwanda Vya Denmark (Danish Industry) (DI).

Kupitia mradi huo, VETA inatangaza nafasi za mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 18 na 35.

**FANI ZINAZOHUSIKA**

1. Umeme wa Viwandani (Industrial Electrical Installation);
2. Umeme wa Majumbani (Domestic Electrical Installation);
3. Ufundi Majokofu (Refrigeration); na
4. Ufundi Ukerezaji vyuma (Fitter Mechanics).

**CHUO KITAKACHOTOA MAFUNZO**

Mafunzo haya yatatolewa kupitia chuo cha VETA KIHONDA.



**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

**VETA MAKAO MAKUU**

Kiwanja Na. 18, Central business Park (CBP)  
S. L. P. 802,  
DODOMA.

+255 755 267 489



## UGHARAMIAJI MAFUNZO

- Ada italipwa na Mradi.
- Mzazi/Mlezi/Mwanafunzi atagharamia chakula na/au malazi wakati wa kuhudhuria mafunzo.

## MUDA WA MAFUNZO

Mafunzo yatafanyika kwa kipindi cha miezi minne darasani na miezi miwili Mafunzo ya vitendo viwandani (Field Attachment).

## SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO

Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:

- Awe ni raia wa Tanzania
- Awe na umri wa kati ya miaka 18 hadi 35
- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au ameajiriwa katika fani husika.

## UTARATIBU WA KUJIUNGA NA MAFUNZO

- Maombi ya kujiunga na mafunzo yapelekwe Chuo cha VETA Kihonda kwa kujaza fomu ya maombi au yawasilishwe kwa barua pepe ifuatayo: [kihondarvtsc@veta.go.tz](mailto:kihondarvtsc@veta.go.tz).
- Fomu za maombi zinapatikana chuoni au kwenye tovuti ya VETA [www.veta.go.tz](http://www.veta.go.tz). Unaweza kuomba fomu kupitia barua pepe ifuatayo: [kihondarvtsc@veta.go.tz](mailto:kihondarvtsc@veta.go.tz)



Dansk Industri



ULANDSSEKRETARIATET – DTDA  
DANISH TRADE UNION DEVELOPMENT AGENCY

**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

**VETA MAKAO MAKUU**

Kiwanja Na. 18, Central business Park (CBP)  
S. L. P. 802,  
DODOMA.



+255 755 267 489

VETA



Wakati wa kurejesha fomu mwombaji anatakiwa aambatanishe nakala ya nyaraka zifuatazo:

- (i) Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha taifa au leseni ya udereva au kadi ya mpiga kura;
- (ii) Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya mtaa/kijiji;
- (iii) Cheti cha kidato cha nne;
- (iv) Barua ya maombi iainishe fani anayoomba; na
- (v) Barua ya Msimamizi/Mwajiri kwa wale walioajiriwa.

## MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NA KUANZA KWA MAFUNZO

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30 Juni, 2023. Usaili wa waombaji utafanyika kati ya tarehe 1 mpaka 10 Julai, 2023.

Mafunzo yanatarajiwa kuanza tarehe 1 Agosti, 2023.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na Chuo kupitia anuani ifuatayo:

MKUU WA CHUO

CHUO CHA VETA KIHONDA

S.L.P 2208, MOROGORO

SIMU: +255 710 63 61 33 AU 0713 23 22 65

BARUA PEPE: kihondarvtsc@veta.go.tz



Dansk Industri



ULANDSSEKRETARIATET – DTDA  
DANISH TRADE UNION DEVELOPMENT AGENCY

**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

**VETA MAKAO MAKUU**


Kiwanja Na. 18, Central business Park (CBP)  
S. L. P. 802,  
DODOMA.



+255 755 267 489

VETA





Imetolewa na,  
MKURUGENZI MKUU  
VETA MAKAO MAKUU  
S. L. P 802, DODOMA  
Barua Pepe: info@veta.go.tz  
Tovuti: www.veta.go.tz



Dansk Industri



ULANDSSEKRETARIATET – DTDA  
DANISH TRADE UNION DEVELOPMENT AGENCY

**UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

**VETA MAKAO MAKUU**

Kiwanja Na. 18, Central business Park (CBP)  
S. L. P. 802,  
DODOMA.



+255 755 267 489

VETA

